

Wanawake wa Ohio wanatoa wito kwa wanawake ulimwenguni, watoto kwa wazee, kusimama imara ili kuukomboa ulimwengu.

Sharon Mehdi aliandika hadithi fupi ya kuvutia kwa mjukuu wake wa miaka mitano.

Iliyosimulia *Ukimya mzito wa mkuatano wa wabibi* ambayo ilituhamasisha sisi sote.

Kifupisho cha hadithi hiyo ni kama kifuatavyo:

Kijana mmoja aliyeleka akifanya kazi katika mgahawa ambaa uliokuwa na dirisha lililotazamana na bustani ya kupumzika ya hadhara alivutiwa na wanawake bibi vizee wawili ambaa walikuwa wamesimama siku nzima kwenye bustani hiyo bila kujisogeza wala kuzungumza. Walikuwa wamevaa mavazi ya kupendeza kama yale yanayovaliwa na wanawake siku za jumapili na walikuwa wakitazama jengo kuu la mji. Kijana huyo aliwaauliza wateja wengine waliokuwepo mgahawani mawazo na mtazamo wao juu ya wanawake hao. Wengi wao walikisia mambo mbali mbali joo yao, lakini mtoto mmoja wa miaka mitano ambaye alikuwepo pale mgahawani alipaza sauti yake na kusema kwamba “mmoja wa wanawake wale ni bibi yake na alikifahamu walichokuwa wakifanya, alisema wamesimama pale ili kuukomboa ulimwengu.” Wanaume wengi waliokuwepo mgahawani hapo walimung`unya maneno na kuzoga na kucheka. Alipokuwa akielekeea nyumbani baada ya kazi, kijana yule aliamua kusimama na kuwaauliza bibi vizee wale na walimjibu kuwa “tupo hapo kuukomboa ulimwengu”

Jioni ile kijana pamoja na wazazi wake walipokuwa wakila chakula cha jioni, kijana aliwaeleza wazazi wake habari ile, ye ye na baba yake walimung`unya mamneno na kuzogazoga lakini mama yake alikaa kimya kabisa. Baada ya chakula cha jioni, mama yake kijana alimpigia simu rafiki zake wa karibu na kuwaelezea habari hiyo.

Asubuhi iliyofuata, kijana yule alipokuwa kazini, alipoangalia dirishani na aliwaona wale bibi vizee pamoja na mama yake, na rafiki wa mama yake na wale wanawake wote waliokuwako pale mgahawani jana yake. Wote walikuwa wamesimama kwa ukimya huku wakitazama jengo kuu na mji. Kwa mara nyingine tena, wanaume waliokuwepo pale mgahawani saa ile walimung`unya maneno na kuzoga na kukebehi kwa kusema maneno kama vile “hauwezi kukomboa ulimwengu kwa kujisimamia tu kwenye bustani ya hadhara kama vile , kwani hiyo ni kazi ya wanajeshi” na “kila mmoja wetu anajua kwamba unahitaji kuwa na mabango na matangazo yanayoelezea juu ya kuukomboa ulimwengu, na sio kujisimamia kwenye bustani tu bila chochote.”

Siku nyingine iliyofuata,wale vibibi waliungwa mkono na wale wanawake ambaa waliokuwepo pale mgahawani pamoja na marafiki zao wengi tu. Hii ilisababisha mwandishi wa habari kuhudhuria katika tukio hilo na kuandika makala juu ya wanawake hao. Siku moja baasa ya makala hayo kuchapishwa,mamia ya wanawake walijitokeza na kuwaunga mkono wanawake wale kwa kusimama kwa ukimya kwenye bustani ile ya hadhara. Meya wa mji akamwamuru mkuu wa polisi kuwaondoa wanawake kwenye mkusanyiko ule kwa sababu walikuwa wakiuaibisha mji. Wakati mkuu wa polisi

alipokuwa akiwaamuru wamawake wale wasambaratike maana hawakuwa na kibali, mmoja wao alimjibu kwamba “ sisi ni watu wa kawaida tu, na tuliosimama kwenye bustani yetu ya hadhara , hatuhutubii wala hatufundishi chochote, sasa kwa nini tuhitaji kibali.” Yule mkuu wa polisi akalifikiria hilo na akakubaliana nalo na akaondoka zake.

Hadithi hii iliishia kwa kuonyesha kuwa jumla ya wanawake 2,223, akiwemo mke wa yule meya wa mji, , mke wa mkuu wa polisi na yule binti wa miaka mitano wakiwa wamesimama kwenye bustani hiyo hadhara kuuokoa ulimwengu.

Tafadhali ungana nasi kwa kusimama kimya kwa dakika tano tu, wakati wa ,saa saba ya mchana (1pm) saa za hapo kwako siku ya Mai 13, 2007, simama kwenye bustani ya hadhara, ama uwanja wa shule ama popote pale panapofaa kukusanyika kuonyesha kukubaliana kwako na ujumbe huu. Tunakuomba pia uwaalike wanaume watakaojali na kuungana na wewe. Tunawaomba pia mlete aina yoyote ya kengele na itakapofika saa saba mchana (1pm) azimisha tukio hili mwanzo na mwisho wa dakika zile tano za ukimya kwa kupiga kengele. Wakati wa kile kipindi cha ukimya, tafadhali fikiria ni jinsi gani wewe binafsi, ama sisi sote kwa pamoja tutawezaje kuupata ulimwengu. Iwapo utahitaji kukaa badala ya kusimama, tafadhali kuwa huru na fanya hivyo . tunatumaini kuwa baada ya hayo yote, wewe na wale uwapendao mnaweza mkazungumza pamoja hitajiko la kibali ulimwenguni humu. Mkuu wa polisi alifikiria na akakubaliana nao na akaondoka zake.

Tunasimama kwa ajili ya watoto na wajukuu na vizazi vingine saba vijavyo mbele yake. Ni ndoto yetu kuwa na dunia ambayo watoto wetu wawe na maji safi na salama ya kunywa, wapumue hewa safi na wawe na chakula cha kutosha. Dunia ambayo watapata elimu ya msingi na huduma za afya wakati wanakua. Dunia ambamo watapata malazi bora, salama na yenye upendo watakapopaita nyumbani. Dunia ambamo hawataishi kwa uoga ama ghasia majumbani mwao, kwenye ujirani wao, mashulen i mwao au haya popote pale ulimwenguni. Hii ndio ile dunia tunayoiota. Hii ndiyo hasa sababu ya kusimama kwetu.
